

HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM



TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA KUKUSANYA USHURU WA MAEGESHO YA MAGARI PAMOJA NA VYOONI KATIKA ENEO LA DCC BUSINESS PARK (MACHINGA COMPLEX)

Meneja wa DCC Business Park (Machinga Complex) anawatangazia wakazi wa Jiji la Dar es Salaam wenye sifa, nafasi ya kazi za katibu Muhtasi (1), Msaidizi wa Ofisi (1), Kukusanya ushuru wa maegesho nafasi (3), Vyooni nafasi (10), Fundi bomba nafasi (1), Wafuatiliaji wa kodi za vizimba (3) na Fundi Umeme (1) . Kazi hii itakuwa ni ya Mkataba wa miezi mitatu na mshahara utalipwa kwa kuzingatia Sheria ya Ajira Cap. 300 "Wage Order" 2013 ambao utakuwa kuanzia Sh.150, 000/= kwa mwezi.

SIFA ZA MWOMBAJI:

- Awe Raia wa Tanzania mwenye umri usiopungua miaka 18 na umri usiozidi miaka 45
- Awe na elimu ya darasa la Saba na kuendelea
- Awe na uwezo wa kutumia "Smart phone" katika miamala ya malipo
- Awe na Uzoefu usiopungua miezi sita kwa kazi anayoiomba.
- Awe mwadilifu na mwaminifu na awe hajawahi kutiwa hatiani kwa kosa la jinai
- Awe na kitambulisho cha Taifa.

MAELEKEZO YA JUMLA

- Waombaji waambatishe vivuli vya vyeti vya taaluma zao pamoja na cheti cha kuzaliwa.
- Kila barua ya muombaji iambatishwe na picha mbili ndogo (Passport size) iliyopigwa siku za karibuni, anuani kamili ya makazi pamoja na namba ya simu.
- Barua ya Maombi iambatishwe na:

- Barua kutoka kwa wadhamini wawili ambao ni watumishi wa Serikali zikiwa na picha "Pass port size" ya hivi karibuni, Anuani kamili ya makazi, pamoja na namba zao za simu.
- Barua ya Utambulisho kutoka kwa Mwenyekiti wa Serikali za Mitaa.
- Wasifu (CV)
- Waombaji watakaokuwa "Shortlisted" watajulishwa kwa njia ya simu tarehe ya usaili.
- Barua ya maombi ya kazi iletwe kwa njia ya mkono katika Ofisi ya Meneja DCC Business Park (Machinga Complex) kuanzia tarehe ya tangazo hili au kwa njia ya posta kupitia anuani tajwa hapo chini kuanzia saa mbili kamili (2:00) asubuhi hadi saa 8:00 mchana. Mwisho wa kupokea maombi ya kazi ni tarehe 16 Novemba, 2020 saa 8:00 mchana.
- Barua zote za maombi zipelekwe kwa Meneja wa DCC Business Park (Machinga Complex)
- **Kila mwombaji anapaswa kutaja nafasi ya kazi anayoomba juu ya bahasha ya maombi.**

Maombi yatunwe kwa Anuani ifuatayo:-

Meneja,
DCC Business Park,
S.L.P. 9084,
Barabara ya Lindi/Shaurimoyo

Tangazo hili pia linapatikana kwenye tovuti ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ambayo ni www.dcc.go.tz



Sipora J. Liana
**MKURUGENZI WA JIJI
HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM**